



Journal of Frontiers in Multidisciplinary Research

Athari Za Kimofonolojia Za Kiswahili Katika Lugha Ya Kisiha

Joan Godwin Kileo

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35110, Dar es Salaam, Tanzania

* Corresponding Author: **Joan Godwin Kileo**

Article Info

E-ISSN: 3050-9726

P-ISSN: 3050-9718

Volume: 06

Issue: 02

July – December 2025

Received: 14-08-2025

Accepted: 16-09-2025

Published: 15-10-2025

Page No: 315-323

IKISIRI

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza athari za Kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha. Utafiti huu una malengo mahususi matatu ambayo ni: kubainisha maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyomo katika lugha ya Kisiha, kueleza athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha, na kufanua sababu za athari za kimofonolojia za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha. Chanzo cha data kilichotumika katika utafiti huu ni uwandani. Data zilikusanywa kwa njia ya mahojiano, hojaji na ushuhudaji kutoka kwa wazee wenye rika la kati ya miaka 50-85 na wanafunzi wa kati ya miaka 10-14 katika wilaya ya Siha. Data zilizopatikana katika utafiti huu zilichambuliwa kwa njia ya maelezo. Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles (1982). Matokeo ya utafiti huu yamedhihirisha kuwa lugha ya Kisiha imeathiriwa na lugha ya Kiswahili hasa katika kipengele cha mofolojia. Aidha, athari za kifonolojia zimejitokeza katika kipengele cha sauti za Kiswahili zilizotumiwa na watoa taarifa wakati walipokuwa wanazungumza Kisiha. Athari hizo ni matumizi ya sauti [z] badala ya sauti [s], sauti [m] badala ya sauti [n], sauti [ch] badala ya sauti [sh] pamoja na udondoshaji wa sauti [h] ya Kisiha. Fauka ya hayo, utafiti huu umeweka bayana sababu za athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha, ambapo miongoni mwa sababu hizo ni elimu, biashara, pamoja na upanuzi wa matumizi ya Kiswahili vijijini. Mwisho ni muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti pamoja na mapendekezo ya tafiti fuatishi ambapo imependekezwa kuwa tafiti zifanyike katika vipengele ambavyo havikushughulikiwa, kama vile sintaksia na semantiki. Aidha, kuna haja ya kufanya tafiti kuhusu mbinu na mikakati ya kuchochea matumizi ya lugha ya Kisiha katika muktadha huu wa kutamalaki kwa lugha ya Kiswahili ili kuweza kudumisha lugha ya Kisiha.

Keywords: Kimofonolojia, Kiswahili, Kisiha, Athari za Lugha

1. Usuli wa Swala la Utafiti

Lugha ni kipengele muhimu sana katika maisha ya binadamu na katika jamii anamoishi. Palipo na watu huwapo pia lugha (Mekacha, 2011) ^[35]. Jamii hutumia lugha ili kuweza kuwasiliana katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Hivyo, lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano katika jamii. Kwa mfano, Kiswahili ni lugha inayotumiwa na Watanzania wengi katika ngazi za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Watanzania wengi hutumia lugha ya Kiswahili katika maeneo yote yaliyo rasmi, kama vile ofisini, mahakamani na shuleni (Chiduo 1999) ^[7]. Pia, katika maeneo yasiyo rasmi lugha hii hutumiwa na Watanzania walio wengi kama vile nyumbani na katika sherehe za kijamii. Matumizi hayo ya lugha ya Kiswahili huwatambulisha Watanzania wengi na jamii pana ya kitaifa (Mekacha, *keshtajwa*). Hivyo, Kiswahili ni lugha ambayo imepanuka na kukua kimatumizi nchini Tanzania na nje ya nchi kama China, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia na Uganda. Lugha ya Kiswahili inatumika pamoja na lugha za kijamii na baadhi ya lugha hizo ni kama vile Kisiha, Kihaya, Kibena, Kinyakyusa, Kijita, Kimeru, Kirangi, Kindengereko, Kihehe, Kingoni, Kimatengo, Kipare, Kirombo, Kizigua, Kifipa, Kikinga, Kizaramo, Kikurya, Kizigua na kadhalika. Mekacha (2011) ^[35] anaeleza kuwa lugha za jamii ni lugha ambazo matumizi yake ni muhimu kwani kila mtu anazitumia katika maisha ya kila siku katika mawasiliano hususan maeneo yasiyo rasmi, hasa vijijini na ni lugha zinazozungumzwa katika jamii mahususi. Halikadhalika, lugha za jamii hutumika katika shughuli mbalimbali kama vile sherehe, mazishi, kilimo na biashara.

Sera ya Utamaduni ya Tanzania (1997) imeweka bayana dhima na maeneo ya matumizi ya kila lugha katika jamii. Nchini Tanzania lugha zimegawanywa kwa kuzingatia dhima, ambapo kuna lugha ya taifa kama vile Kiswahili, lugha za kigeni kama

vile Kiingereza, Kiarabu, Kijerumani na Kichina na lugha za jamii kama vile Kisiha, Kiwoso, Kibena, Kikinga, Kimeru, Kimachame, Kinyakyusa na Kikurya kwa kutaja chache. Lugha ya Kiswahili hutumika katika mawasiliano rasmi hususan bungeni, katika mahakama za mwanzo, shuleni na ofisini.

Msanjila (1999) ^[41] anaeleza kuwa kutokana na upana wa matumizi yake, lugha ya Kiswahili imeenea sana kuliko lugha za jamii. Kupanuka kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili hadi vijijini hususan katika ngazi mbalimbali, kumechangia kwa kiasi kikubwa kuathiriwa kwa lugha za jamii, ikiwemo Kisiha.

Kwa mujibu wa Dressler (1988) ^[10] kutokana na lugha kutumika kwa muda mrefu na mwanadamu ndivyo historia ya kuathiriwa kwa lugha huongezeka katika nyanja tofautitofauti kama vile fonolojia, mofolojia, sintaksia pamoja semantiki. Vilevile, Chimera (1999) ^[8] anafafanua kuwa kuathiriwa au kuathiri hutokea pale pengo la kimawasiliano linapotokea baina ya lugha moja na nyingine. Pengo hilo hutokea pale lugha inapokosa maneno ya kutosha pamoja na tofauti za miundo ya ndani ya lugha husika. Kwa hiyo, ili pengo hilo lizibwe hasa katika mawasiliano, lugha moja huweza kukopa au kutohoa maneno kutoka katika lugha hizo nyingine. Hivyo, kukopa na kutohoa maneno kutoka katika lugha nyingine kunachangia lugha kuathiriwa na miundo ya nje kama sauti na msamiati na miundo ya ndani ya lugha nyingine. Mukuthuria (2004) ^[43] anafafanua kuwa lugha inapoathiriwa huwa inalenga kujiiimarisha na kujitosheleza na inapoathiri huwa inalenga kuimarisha na kutosheleza lugha inayopokea athari.

Kwa mujibu wa Kapinga (1983) ^[17] akinukuliwa na Mramba (2015) ^[40] anaeleza kuwa athari za lugha moja katika lugha nyingine zinaweza kujidhihirisha katika fonolojia ya lugha inayohusika. Hali hii inaweza kuonekana pale lugha moja inapochukua baadhi ya sauti kutoka lugha nyingine. Kapinga (*keshatajwa*) anabainisha namna lugha ya kwanza inavyoathiri Kiswahili kama lugha ya pili katika matamshi yake, kwa mfano, Kipare: *thithi* badala ya *sisi*, *thamaki* badala ya *samaki*, Kikurya: *kurara* badala ya *kulala*, *mahari* badala ya *mahali*.

Tafiti kuhusu athari za lugha mbalimbali zimefanywa na wataalamu mbalimbali. Miongoni mwa watafiti hao ni Luka (2012) ^[26] ambaye alichunguza kuhusu mwingiliano wa matumizi ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kimeru na athari zake. Matokeo ya utafiti huo yanadhihirisha kuwa kuna athari za kifonolojia ambazo husababishwa na tofauti ya idadi ya konsonanti katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kimeru. Pia, alibaini kuwapo kwa athari za msamiati katika lugha ya Kimeru kulikosababishwa na kukopa maneno mengi kutoka katika lugha ya Kiswahili.

Lusanja (2014) ^[27] amechunguza kuhusu athari za Kiswahili katika msamiati wa Kiwanji. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa kuna idadi kubwa ya msamiati wa Kiswahili katika Kiwanji. Vilevile, sababu zilizobainika ambazo huchangia athari hizo ni ukopaji wa msamiati wa Kiswahili ambao hutumika katika lugha ya Kiwanji. Hivyo, ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili huathiri lugha ya Kiwanji kutokana na mwingiliano wa msamiati.

Mramba (2015) ^[40] alichunguza kuhusu athari ya lugha ya Kirombo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Matokeo ya utafiti wake yanaonesha kuwa kuna athari kubwa wanayoipata wanafunzi wa Kirombo katika vipengele vya fonolojia na mofolojia wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Pamoja na utafiti huo wa Mramba

kuonesha athari za kifonolojia na kimofolojia za lugha ya Kirombo katika lugha ya Kiswahili, utafiti huo haukuchunguza athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha kwa kuwa halikuwa lengo lake la utafiti.

1.1. Tatizo la Utafiti

Jamii mbili tofauti zinazozungumza lugha tofauti zinapokaa pamoja zinaathiriana katika nyanja mbalimbali za kiutamaduni na lugha ikiwemo, (Mekacha, 2011) ^[35]. Katika lugha, athari hizo hujitokeza katika vipengele vya fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Aidha, kazi chache za utafiti zilizofanywa kuhusu kipengele hiki, zinaonesha kuwa lugha ya Kiswahili imeziathiri lugha za Kibantu na lugha za Kibantu zimeathiri lugha ya Kiswahili. Chanzo cha athari hizo ni ukaribu uliopo baina ya lugha hizo. Hata hivyo, tafiti hizo hazijashughulikia kipengele cha athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha, kwa kubainisha maneno ya Kiswahili yaliyomo katika lugha ya Kisiha na athari za kimofolojia na kifonolojia za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha.

1.2. Malengo Mahususi

1. Kubainisha maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyomo katika lugha ya Kisiha.
2. Kueleza athari za kifonolojia za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha na
3. Kufafanua sababu za athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha.

2. Mapitio Ya Tafiti Zilizotangulia Na Kiunzi Cha Nadharia

2.1. Dhana ya Neno

Spencer (1991) ^[48], anaeleza kuwa neno ni dhana changamani; hivyo siyo rahisi kulifasili kwa kutumia kigezo kimoja. Neno linaweza kufasiliwa kwa kuzingatia kigezo cha kifonolojia, kisemantiki, kisintaksia, kiothografia na kileksika. Wataalamu mbalimbali wamefasili dhana ya neno. Kwa mfano, TUKI (2013) ^[53] wanafasili neno kwa kutumia kigezo cha kimofonolojia kuwa neno linaweza kufafanuliwa katika misingi ya kiumbo-sauti (kwa kuchunguza sauti zinazounda neno zima), kiothografia (kwa kuchunguza herufi zinazotumika katika kuandika umbo lake) na kisarufi (kwa kuchunguza kile kinachowakilishwa na umbo husika katika lugha). Katika utafiti huu, neno limefasiliwa kwa kigezo cha kifonolojia ambapo kwa maelezo ya TUKI (1990) ^[51], neno ni silabi zinazotamkwa au kuandikwa. Silabi hizo huwa ni tofauti baina ya lugha moja na nyingine. Hivyo, neno ni dhana muhimu katika lugha yoyote. Aina za maneno zimeainishwa na wataalamu kwa mitazamo tofautitofauti. Kwa mitazamo hiyo, idadi ya aina za maneno pia zimetofautiana kutoka mtaalamu mmoja na mwingine. Mfano, mwanasarufi wa Kigiriki Dionysius Trax kama alivyonukuliwa na Baker (2003) ^[3] aliainisha aina nane za maneno ambazo ni nomino, kitenzi, kibainishi, kihisishi, kibatala, kielezi na kiunganishi kutokana na muundo wa lugha ya Kigiriki. Kwa upande wa lugha ya Kiswahili, maneno yameainishwa katika kategoria mbalimbali. Mathalani, Kapinga (1983) ^[17] anaainisha aina saba za maneno ambazo ni majina, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, vielezi, vihusishi na viingizi. Kihore *na wenzie* (2003) ^[20] wanaainisha aina saba za maneno, yaani vitenzi, viunganishi, vielezi, viwakilishi, vivumishi, vihusishi na viingizi.

Hata hivyo, Kihore *na wenzie* (2003) ^[20] wanatofautiana na Kapinga (1983) ^[17] katika baadhi ya istilahi anazotumia katika uainishaji wake. Kihore *na wenzie* (2003) ^[20] wanatumia istilahi kama vile nomino, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, vielezi, viunganishi, na viingizi. Kapinga (1983) ^[17] anatumia istilahi kama vile majina, vivumishi, viwakilishi, vitenzi, vielezi vihusishi na viingizi. Aidha, katika utafiti huu uainishaji wa maneno katika kategoria zake umezingatia mkabala kimuundo, Kihore *na wenzie* (2003) ^[20]. Uainishaji huu ni muhimu kwa kuwa mtafiti ameweza kuyapanga maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyomo katika lugha ya Kisiha kwa kuzingatia kategoria, ili kukamilisha azma ya lengo mahususi la kwanza katika utafiti huu.

2.2. Dhana ya Fonolojia

O'Grady *na wenzie* (1997) wanafasili fonolojia kuwa ni taaluma ya uchanganuzi na ufafanuzi wa miundo na uamilifu wa sauti katika lugha. Anaendelea kueleza kuwa kipengele muhimu katika lugha ni fonimu. Kipengele hiki cha fonimu kinashughulikia mfumo wa sauti katika lugha na jinsi sauti hizo zinavyoingana ili kuunda maneno yanayokubalika katika lugha. Kila lugha ina utaratibu wake wa kupangilia vitamkwa ambavyo hutumika katika kuunda silabi, mofimu na neno. Aidha, lugha zinaweza kuathiriana kutokana na matumizi ya lugha nyingine, athari zinaweza kujitokeza katika fonolojia ya lugha yenyewe. Athari za kifonolojia zinajitokeza pale ambapo wazungumzaji wa lugha Y wanapotumia sauti ya lugha X, kwa mfano, baadhi ya Wasiha wanapotumia sauti [z] ya lugha ya Kiswahili mahali ambapo walitakiwa kutumia sauti [s] ya lugha ya Kisiha. Kwa mfano, neno *sawadi* wao wanatamka *zawadi* kutokana na athari ya lugha ya Kiswahili (taz. 4.3.1). Kutokana na mfano huu inaonesha kuwa kuna athari za kifonolojia za Kiswahili zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa lugha ya Kisiha.

2.3. Dhana ya Mofolojia

Katamba (1993) ^[18] anafasili mofolojia kuwa ni taaluma inayohusiana na uchanganuzi na ufafanuzi wa muundo wa maneno na uamilifu wa kisarufi wa sehemu mbalimbali za maneno. Kipashio cha msingi katika mofolojia ni mofimu. Kwa kawaida maneno yote huwa ni matokeo ya kuweka vipashio pamoja na vipashio hivi hudokeza nafsi, njeo, umoja na wingi. Vilevile, kila lugha ina utaratibu wake wa kupachika vipashio hivi katika maumbo ya maneno. Katika utafiti huu mofolojia ni muhimu katika kubainisha maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyopo katika lugha ya Kisiha.

2.4. Dhana ya Mofofonolojia

Ogden (2009) ^[45] anaeleza kuwa mofofonolojia ni muunganiko wa taaluma za aina mbili za kiisimu, ambazo ni taaluma ya fonolojia na mofolojia. Anaendelea kueleza kuwa mofofonolojia ni taaluma inayojishughulisha na uchanganuzi na uainishaji wa vipengele vya kifonolojia vinavyoathiri maumbo ya mofu katika mfuatano wake. Hivyo, mofofonolojia inahusika na uchanganuzi wa vipengele vya kifonolojia ndani ya maumbo ya mofolojia. Aidha, Massamba (2010) ^[31] anaeleza kuwa mofofonolojia ni sehemu ya isimu ambayo inatumia mofolojia kuelezea tofauti fulani za kifonolojia. Kwa hiyo, kuwepo kwa mchakato wa kimofofonolojia ni kutokana na mabadiliko ya sauti ambazo hazikuweza kufafanuliwa kwa kutumia kipengele cha kifonolojia pekee au utaratibu wa kimofolojia pekee. Katika utafiti huu mofofonolojia ni muhimu kwa kuwa imetumika katika kuelezea mabadiliko ya sauti ambayo yapo katika

fonolojia na maneno ambayo ni mofolojia.

2.5. Mapitio mbalimbali kuhusu Kuathiriana kwa Lugha

Mekacha (2011) ^[35] anaeleza kwamba kwa kawaida lugha huathiriana. Anaendelea kueleza kuwa kuathiriana kwa lugha ni jambo lisiloweza kuepukika kwa lugha mbili au zaidi hasa pale zinapotumika katika eneo moja. Kwa kawaida lugha huathiriana kwa sababu kuna baadhi ya sauti zinaweza kutumika pamoja kwa watumiaji wa lugha zote. Pia, lugha huweza kukopa maneno kutoka lugha nyingine ili kukidhi haja ya lugha. Ukopaji wa maneno hayo huweza kuhatarisha lugha inayopokea maneno kwa kupoteza maneno yake ya asili. Aidha, Zawazi (1979) akichunguza kuhusu athari ya lugha ya Kiarabu katika Kiswahili, alibaini kuwa Kiswahili kimeathiriwa na Kiarabu hususan katika maneno ya mkopo. Aidha, anaeleza kuwa kukopa maneno kutoka katika lugha nyingine husababisha athari za kimuundo na kimsamiati kwa lugha zinazohusika. Baadhi ya msamiati hubadilika katika matamshi; wakati mwingine maneno mapya huzuka ili kukidhi mahitaji. Vilevile, Zawazi (*keshatajwa*) anasisitiza kwamba haiwezekani lugha moja kuingiliana na lugha nyingine pasipo kuathiriana.

Naye Thomason (2001) ^[49] akichunguza kuhusu lugha ya Kiingereza, alibaini athari ambazo zilijitokeza kutokana na ukopaji wa maneno mengi ya Kifaransa. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa Kiingereza kina asilimia 75 ya maneno ya Kifaransa. Hivyo, kutokana na matokeo ya utafiti huo lugha ya Kiingereza imethiriwa katika vipengele vyote vya kimuundo ambavyo ni mofolojia, fonolojia, sintaksia na semantiki. Kwa upande mwingine Thomason (*keshatajwa*) akiendelea kuchunguza athari ya lugha za kikabila huko Paraguay, alieleza kuwa kuathiriana kwa lugha kunatokana na kuingiliana kwa wazungumzaji wanaotumia lugha zaidi ya moja katika mazingira mamoja. Aidha, anaeleza kuwa lugha za makabila huko Paraguay zimeathiriwa na lugha ya Guarani zinazozungumzwa Pwani ya Spanish na idadi kubwa ya watu na huchukulia kama lugha ya taifa. Hivyo, kutokana na mwingiliano huo lugha za kikabila za Paraguay ziko hatarini kutoweka kutokana na wanajamii kutumia lugha nyingine. Hivyo, kuathiriana kwa lugha ni suala ambalo haliwezi kuzuilika hasa pale lugha zaidi ya moja zinapotumika katika mazingira ya aina moja.

Kwa upande mwingine, Arab (2015) ^[2], alitafiti kuhusu athari ya Kifaransa katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza huko Algeria. Matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa lugha ya Kiingereza kama lugha ya kigeni imeathiriwa na Kifaransa kutokana na kukopa maneno mengi kutoka katika lugha hiyo. Kwa upande mwingine, kuathiriwa huko kwa lugha ya Kiingereza, kulitokana na ukaribu wa matumizi ya lugha hizo. Aidha, lugha ya Kifaransa ni lugha iliyotumiwa kwa muda mrefu tangu enzi za ukoloni huko Algeria, hivyo ni lugha ambayo inatumikiwa kwa kiasi kikubwa. Matokeo ya utafiti huo yameweka bayana maneno ya Kiingereza yaliyokopwa kutoka katika Kifaransa ambayo ni "*salad*", "*arest*", "*jury*" na "*basin*". Arab (*keshatajwa*) anaeleza kuwa matumizi ya maneno ya Kifaransa yamechangia athari katika lugha ya Kiingereza katika vipengele vya fonolojia na mofolojia katika lugha ya Kiingereza. Hivyo kutokana na matokeo ya utafiti huo uliofanyika huko Algeria ni wazi kuwa lugha zinapotumika katika mazingira mamoja huweza kuathiriana kutokana na kuchanganya maneno.

Rubanza (1979) ^[46] alifanya utafiti kuhusu athari ya lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kihaya. Katika utafiti huo alibaini

kuwa lugha ya Kihaya iliathiriwa na Kiswahili. Athari hizo zilijipambanua katika vipengele vya matamshi na msamiati. Kwa mujibu wa utafiti huo athari hizo zilisababishwa na elimu, ambapo Wahaya wasomi walipenda kujipambanua dhidi ya wengine wasiosoma. Kutokana na hali hiyo basi, baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu, kwa mujibu wa utafiti huo, yalielekea kufanana na maneno ya Kihaya. Akithibitisha hoja yake hiyo Rubanza (1979)^[46] anatoa mifano ifuatayo:

Kihaya	Kiswahili
eshuule	shule
euma	uma
edafutari	daftari

Chanzo: Rubanza (1979: 119)

Katika kazi hiyo, kama mfano (2) unavyoonesha hapo juu, Rubanza (*keshatajwa*) alijiegemeza katika maumbo ya maneno na matamshi. Alibaini kuwa msamiati wa Kihaya ulikuwa na athari za lugha ya Kiswahili na ulielekea kufanana na ule wa Kiswahili. Kauli hiyo ina mashiko hasa tukiitazama kwa makini data inayotolewa na Rubanza (1979)^[46], kwani maneno yanafanana sana. Utafiti wa Rubanza (*keshatajwa*) ulitofautiana na kazi hii kwa vile ulikuwa na mwelekeo wa mofolojia na haukushughulikia ngazi ya kimofonolojia kwa kina. Hivyo, utafiti huu umechunguza kuhusu athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha.

Aidha, Mochiwa (1979)^[39] amechunguza athari za Kiswahili katika lugha ya Kizigua nchini Tanzania, lugha inayozungumzwa katika wilaya ya Handeni, mkoa wa Tanga. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa Wazigua waliathiriwa na lugha ya Kiswahili, hasa katika vipengele vya fonolojia, semantiki, sintaksia na mofolojia. Sababu zinazoelezwa na Mochiwa (*keshatajwa*) kama chanzo cha kuathiriwa huko ni elimu na kazi. Wafanyakazi walipendelea sana kuzungumza Kiswahili kuliko lugha za asili. Vilevile, sababu nyingine ni kama vile elimu, uhamiaji, wingilugha pamoja na mwingiliano wa wanajamii tofautitofauti. Kwa upande wa kipengele cha fonolojia, Mochiwa (1979)^[39] alizingatia matamshi ya sauti za Kizigua na aligundua kuwepo kwa mabadiliko katika baadhi ya sauti katika lugha hiyo. Mabadiliko hayo ni pamoja na sauti [l] ya Kizigua kutamkwa kama [r] ya Kiswahili. Ili kushadidia hoja hii Mochiwa ametoa mifano ifuatayo:

Kiswahili Sanifu	Matamshi ya Kizigua
/Madarasa/ (madarasa)	/madalasa/ (madalasa)
/Mara/ (mara)	/mala/ (mala)
/Urafiki/ (urafiki)	/ulafiki/ (ulafiki)

Chanzo: Mochiwa (1979: 100)^[39]

Kwa kuchunguza mifano katika (3) ni wazi kuwa matamshi ya Kizigua yanatumia sauti [l] ya Kiswahili badala ya [r] ya Kizigua kutokana na lugha ya Kizigua kuathiriwa na Kiswahili sanifu. Hali hiyo husababisha sauti hizo kutamkwa kama zinavyotamkwa katika Kiswahili. Matokeo ya utafiti wa Mochiwa yana mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kuwa yanaonesha lugha ya Kizigua ilivyoathiriwa na lugha ya Kiswahili. Mochiwa (*keshatajwa*) ameweka bayana mambo yanayosababisha lugha ya Kiswahili kuathiri Kizigua. Hata hivyo, Mochiwa (*keshatajwa*) hakuchunguza athari za kimofonolojia za lugha za Kiswahili katika lugha ya Kisiha jambo ambalo utafiti huu umeshughulikia.

Fauka ya hayo, utafiti mwingine ni ule wa Khamis (2012)^[19] ambao umechunguza athari za matamshi ya msamiati wa Kiswahili sanifu katika Kimakunduchi. Utafiti huu

ulibainisha vipengele mbalimbali vinavyosababisha athari za kimatamshi katika lugha. Sababu zinazoelezwa ni pamoja na mwingiliano (mtagusano) unaosababishwa na shughuli za kiuchumi na kisiasa, sababu za kijiografia, kuenea kwa vyombo vya habari, mtazamo hasi miongoni mwa watumiaji wa lahaja ya Kimakunduchi pamoja na matumizi ya maneno ya Kiswahili sanifu badala ya Kimakunduchi. Matokeo ya utafiti wa Khamis (*keshatajwa*) yanaonesha kuwa lahaja ya Kimakunduchi imeathiriwa na Kiswahili sanifu katika baadhi ya sauti za maneno ya asili. Athari ya Kiswahili sanifu imesababisha Kimakunduchi kutumia sauti za Kiswahili sanifu katika matamshi ya baadhi ya maneno ya lahaja hiyo. Sauti ambazo zimebadilika kutokana na athari ya Kiswahili sanifu katika lahaja ya Kimakunduchi ni sauti [v] badala ya sauti [p]; [ʃ] badala ya sauti [s] na [t] badala ya sauti [s] katika nafasi sawa katika maneno yenye maana sawa na maumbo yanayokaribiana na maumbo ya Kimakunduchi na Kiswahili sanifu.

Utafiti huo umeonesha namna lahaja ya Kimakunduchi ilivyoathiriwa na Kiswahili sanifu. Hii inaonesha dhahiri kuwa lugha mbili zinapokutana huathiriana katika vipengele vya kiisimu. Utafiti huu wa Khamis (*keshatajwa*) una mchango mkubwa katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu amechunguza masuala ya kuathiriana kwa lugha za nasaba moja ambazo ni Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu wa sasa unachunguza maneno ya Kiswahili yaliyomo katika lugha ya Kisiha. Pia utafiti, wa Khamis ulifanyika Zanzibar lakini utafiti huu umefanyika Tanzania Bara.

Aidha, utafiti mwingine unahusu athari ya lugha za jamii katika mkoa wa Mara nchini Tanzania (Massamba, 1986)^[29]. Katika kazi hiyo Massamba anabainisha kuwa athari za lugha nikutokana na mwingiliano wa lugha zaidi ya moja zinazotumiwa wakati wa mawasiliano katika mazingira mamoja. Massamba (*keshatajwa*) anaeleza kuwa kuenea kwa lugha ya Kiswahili bara kulitokana na Waarabu kutumia lugha ya Kiswahili kuwasiliana na watu wa bara. Madai ya Massamba (*keshatajwa*) ni kwamba katika shughuli za Wamisionari na harakati za ukombozi, lugha iliyotumika ni Kiswahili. Hata hivyo, alibaini kuwa kupanuka kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili kulichangia kuathiriwa kwa lugha za eneo la Mara.

Kwa hiyo, athari za kifonolojia huweza kujitokeza katika msamiati, matamshi na sauti. Katika athari za sauti, anaeleza kwamba kuna matumizi ya sauti [r] badala ya [l] katika lugha za jamii za mkoa wa Mara. Pamoja na hayo, anabainisha sababu mbalimbali zilizochangia kuathiriana kwa lugha ya Kiswahili na lugha za Mara kuwa ni hadhi, uhamiaji, wingilugha, elimu na matumizi ya Kiswahili ambacho siyo sanifu. Matokeo ya utafiti wa mtaalamu huyu yana manufaa katika utafiti huu. Kwanza, yamesaidia katika uteuzi wa mada ya utafiti kwa sababu Massamba (1986)^[29] alijiegemeza katika kuchunguza kuathiriana kwa lugha za eneo la Mara na lugha ya Kiswahili, katika ngazi ya kileksika na kisemantiki. Hivyo, utafiti huu umechunguza athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha.

Bosha (1993)^[5] katika utafiti wake anachunguza kuhusu Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na kamusi Thulathiya ya Kiswahili-Kiarabu-Kiingereza. Katika utafiti wake anajaribu kuelezea jinsi Kiarabu kilivyokiathiri Kiswahili katika matumizi ya kila siku. Madai ya Bosha (*keshatajwa*) ni kuwa kuathiriwa huko kwa Kiswahili ni matokeo ya kukopa maneno kutoka katika lugha ya Kiarabu na jinsi maneno hayo yanavyotumiwa katika mfumo wa

lughu ya Kiswahili. Hivyo, utafiti wa Boshu (*keshatajwa*) unadhahirisha kwamba ukopaji wa maneno kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine una athari katika vipengele mbalimbali kama vile mofolojia, fonolojia, sintaksia na semantiki. Aidha, Boshu (*keshatajwa*), anakisia kwamba katika lugha ya Kiswahili kuna asilimia 43% ya maneno kutoka katika lugha ya Kiarabu. Boshu (*keshatajwa*) alionesha baadhi ya maneno ya Kiarabu yaliyoingia katika Kiswahili ni “*kalamu*” na “*fahari*”. Licha ya hayo, Boshu (*keshatajwa*) anaendelea kueleza kuwa lugha hupokea maneno ya kigeni ili kuweza kuelezea dhana ngeni. Pia, dhana ngeni zinazoathiri Kiswahili ni zile zinazohusiana na utamaduni, mifumo ya siasa na jamii, sheria, biashara na utabibu.

Akitoa mifano katika kipengele cha utamaduni, Boshu (*keshatajwa*) ametumia mifano ya maneno kutoka katika sheria kama vile *hakimu* na *sheria*. Kwa upande wa biashara, anatumia mifano ya maneno kama vile *faida* na *hasara*. Katika utabibu anabainisha maneno kama vile *maradhi*, *tiba*, *zahanati* kwa uchache. Utafiti wa Boshu (*keshatajwa*) unadhahirisha kwamba ukopaji wa maneno kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine una athari katika vipengele mbalimbali kama vile mofolojia, fonolojia, sintaksia na semantiki. Hivyo, tofauti na utafiti wa Boshu (*keshatajwa*) utafiti huu umechunguza kuhusu athari za kimofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha.

Naye Mukuthuria (2004) [43] alichunguza kuhusu kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru kwa kutumia mfano kutoka kwa wanafunzi wa Tigania, nchini Kenya. Utafiti wake uliegemea katika fonolojia na mofolojia. Mukuthuria (*keshatajwa*) katika utafiti wake aligundua kuwa lugha za Kiswahili na Kitigania zimeathiriana katika vipengele vya fonolojia. Matokeo yanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kitigania zina mifumo tofauti ya kifonolojia pale fonimu zinazotumika. Pia, kuna michakato mingine ya kifonolojia ikiwemo: ubadilishaji wa sauti, uchopekaji na udondoshaji ambayo inajitokeza katika lugha ya Kitigania. Mukuthuria (*keshatajwa*) anaeleza kuwa sauti [h] haipatikani kabisa katika lugha ya Kitigania, tofauti na sauti nyingine za konsonanti ambazo zina ukaribu wa kifonetiki ambazo huweza kuchukua nafasi ya sauti hizo. Hivyo basi, wazungumzaji wa Kitigania hudondosha sauti [h] katika mazingira yoyote. Kwa mfano:

Kiswahili Sanifu	Kitigania
/hana/	/φana/
/kuhama/	/kuφama/
/sitawahi/	/sitawaφi/

Chanzo: Mukuthuria (2004: 98) [43]

Kutokana na mifano iliyotolewa na Mukuthuria (*keshatajwa*) ni dhahiri kuwa watumiaji wa lugha ya Kitigania hudondosha sauti [h] ili matamshi yaendane na mfumo wa lugha ya Kitigania. Matokeo yanaonesha kuwa lugha za Kiswahili na Kitigania zina mifumo tofauti ya kifonolojia pale fonimu zinazotumika. Utafiti wa Mukuthuria (*keshatajwa*) ni tofauti na utafiti huu kwakuwa ulijikita katika kuchunguza kuathiriana kwa lugha ya Kiswahili na Kitigania. Aidha, uchunguzi huu ulijikita katika ngazi ya mofolojia na fonolojia. Hivyo, utafiti huu umejikita katika kuchunguza

athari za Kiswahili katika lugha ya Kisiha katika ngazi za mofolojia na fonolojia.

Kazi nyingine ni ile ya Kadenge (2003) [16] inayojaribu kutazama namna utamkaji wa matamshi ya Kiingereza ulivyoathiriwa na matamshi ya Kishona cha Zimbabwe. Katika kazi hiyo, kama Kadenge anavyoeleza, msisitizo mkubwa umewekwa katika uchanganuzi wa matamshi ya kipengele cha irabu unganifu katika Kiingereza zinavyotamkwa na Wamashona. Katika kazi hiyo Kadenge (*keshatajwa*) alibaini kuwepo kwa sababu kadhaa ambazo kimsingi ndizo zinazoibua athari hizo za kimatamshi kwa upande wa Kiingereza. Kwanza, Kiingereza ni lugha ya kigeni ambayo Mmashona hujifunza baada ya kuwa amekwishakipata Kimashona. Pili, kuwepo kwa tofauti za kiisimu hasa zile zinazohusisha mfumo wa irabu. Kiingereza kina irabu unganifu wakati Kimashona hakina irabu unganifu. Kutokana na upungufu huo basi, msemaji wa Kiingereza ambaye ni Mmashona katika matamshi yake analazimika kuchopeka irabu fulani katika matamshi ya Kiingereza. Kwa mfano:

Matamshi ya Kiingereza	Kiingereza-Kimashona
/peI/	/peI/ ‘lipa’
/pleI/	/pejI/ ‘cheza’

Chanzo: Kadenge (2010: 55)

Kadenge (*keshatajwa*) anaeleza kuwa lugha ya Kiingereza nchini Zimbabwe hupitia katika maandiko, yaani vitabu na walimu wazawa ambao kimsingi wamekwishaathiriwa na vipengele vya matamshi ya lugha zao za awali, Kimashona kikiwa miongoni mwazo. Madai ya Kadenge (*keshatajwa*) ni kwamba athari za matamshi ya Kimashona katika matamshi ya Kiingereza zimedhihirika. Sababu nyingine kwa mujibu wa Kadenge (*keshatajwa*) ni ile ya upungufu wa wataalamu wa kufundisha matamshi ya Kiingereza. Uchunguzi huu ulikuwa na manufaa kwa kuwa ulizingatia kuathiriana kwa lugha. Kutokana na utafiti wa Kadenge ni wazi kuwa lugha ya Kimashona, imeathiri lugha ya Kiingereza kwa sababu zote zinatamika katika mazingira hayohayo katika mawasiliano. Hata hivyo, utafiti huu ulikuwa tofauti na utafiti wa Kadenge kwa kuwa alichunguza namna lugha ya Kibantu (Kimashona) ilivyoathiri lugha ya Kigeni (Kiingereza). Aidha, hakushughulikia lugha za Kibantu zinavyoathiriana kama zilivyoshughulikiwa katika utafiti huu. Aidha, Kadenge katika utafiti wake alichunguza athari za kifonolojia pekee ilhali utafiti huu umejikita katika kuchunguza vipengele vya fonolojia na mofolojia.

Utafiti mwingine ni ule uliofanywa na Luka (2012) [26], ambao uliangazia mwingiliano wa matumizi ya lugha kati ya Kiswahili na lugha ya Kimeru na athari zake katika lugha hizo. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa kuna athari za kifonolojia katika lugha ya Kimeru katika lugha ya Kiswahili. Luka (*keshatajwa*) anaeleza kuwa athari hizo husababishwa na tofauti ya idadi ya konsonanti katika lugha za Kiswahili na Kimeru. Kukosekana kwa baadhi ya sauti hizo za lugha ya Kiswahili kumewaathiri wazungumzaji wengi wa Kimeru pindi wanapozungumza Kiswahili sanifu. Wazungumzaji wa Kimeru hutumia sauti mbadala ambazo zipo katika lugha ya Kimeru wakati wakizungumza Kiswahili. Sauti zilizobainishwa ni sauti [a] badala ya sauti [h] na [s] badala

ya sauti [z] ya Kiswahili sanifu. Mifano ifuatayo inashadidia hoja hii:

Kiswahili Sanifu	Matamshi ya Kimeru
Bahasa imeletwa	Baasha imeletwa
Leta sahani	Beta saani
Halafu	Alafu uje

Chanzo: Luka (2012: 52) ^[26]

Kiswahili Sanifu	Matamshi ya Kimeru
Amevaa kanzu	Amevaa kansu
Nunua uzi	Nunua usi
Yuko zamu leo	Yuko samu

Chanzo: Luka (2012: 50) ^[26]

Pia, Luka (2012) ^[26] katika utafiti wake, amebaini kuwepo kwa athari ya msamiati ambapo anaeleza kuwa lugha ya Kimeru imeathiriwa na lugha ya Kiswahili kutokana na kukopa maneno mengi kutoka katika lugha ya Kiswahili. Msamiati uliokopwa ni kama vile *mbunge, kalamu, shule, ufunguo, simu, sukari, mashine, bendera, malaika*. Matokeo ya jumla ya utafiti huu yamedhihirisha athari zinazojitokeza katika lugha za Kiswahili na Kimeru. Athari hizo ziko hususan katika kipengele cha sauti (fonolojia) na kipengele cha (msamiati) mofolojia. Kutokana matokeo ya utafiti huo ni wazi kuwa lugha mbili zinapotumika katika jamii hazikosi kuathiriana katika vipengele vya kiisimu ambavyo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Tofauti na utafiti huo, utafiti huu wa sasa umeshughulikia athari za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha kwa kuzingatia vipengele viwili vya kiisimu ambavyo ni fonolojia na mofolojia.

Kwa upande mwingine, Lusanja (2014) ^[27] alitafiti kuhusu athari za Kiswahili katika msamiati wa Kiwanji. Mtafiti alibaini kuwa Kiswahili kimeathiri Kiwanji kwa sababu ya kutumika katika mazingira mamoja katika mawasiliano ya kila siku. Alibainisha sababu za lugha ya Kiswahili kuathiri lugha ya Kiwanji kuwa ni mwingiliano wa kimatumizi baina ya Kiswahili na Kiwanji, baadhi ya maeneo kutokuzungumza Kiwanji, shughuli za kijamii na kibiashara pamoja na ukopaji wa msamiati kutoka katika lugha ya Kiswahili. Akithibitisha hoja yake hiyo Lusanja (*keshatajwa*) anatoa mifano ifuatayo:

Nomino za Mkopo	Unukuzi katika Kiswahili
Ifilimbi	Filimbi
Egale	Gari
Tala	Taa

Chanzo: Lusanja (2014: 31) ^[27]

Aidha, kutokana na kazi hiyo ya Lusanja (*keshatajwa*) ni dhahiri kuwa lugha ya Kiwanji iko hatarini kupotea kutokana na matumizi ya msamiati wa Kiswahili. Matokeo haya yanatupa mwangaza kwamba lugha mbili zinapotumika katika eneo moja hazina budi kuathiriana. Mtafiti amechunguza athari ya Kiswahili katika Kiwanji kwa kujiegemeza katika msamiati. Utafiti huu wa sasa ulikuwa tofauti na Lusanja (*keshatajwa*) kwa kuchunguza athari za Kiswahili katika lugha ya Kisiha, kwa kujiegemeza katika vipengele vya mofolojia na fonolojia.

Utafiti mwingine ulifanywa na Mramba (2015), aliyechunguza kuhusu athari za lugha ya Kirombo katika ujifunzaji wa lugha ya pili ambayo ni Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kuna athari kubwa wazipatazo wanafunzi Warombo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili ambazo ni athari za kimatumishi. Athari hizo za matamshi zimejibainisha katika matumizi ya sauti za

maneno ya Kiswahili yenye sauti ambazo zipo katika mfumo wa sauti za Kirombo; hivyo, wanafunzi hutumia sauti za lugha ya Kirombo wakati wanapozungumza Kiswahili. Aidha, Mramba (2015) ^[40] aligundua athari nyingine za kifonolojia ambazo zimejidhihirisha katika udondoshaji wa sauti [h] ambazo zinaweza kuwa mwanzoni, au katikati ya neno. Udondoshaji huo hujitokeza sauti [h] inapofuatiwa na irabu yoyote. Kwa mfano:

Lugha ya Kiswahili	Lugha ya Kirombo
Halafu	ɸalafu
Kahawa	ɸkaawa
Haupo	ɸayupo

Chanzo: Mramba (2015: 69)

Mramba (2015) ^[40] amebaini kuwa katika lugha ya Kirombo sauti [h] hudondoshwa katika mazingira yoyote, iwe mwanzoni au katikati mwa neno. Utafiti huo ni tofauti na utafiti huu kwa kuwa ulijiegemeza katika kuchunguza athari za kifonolojia na kimofolojia kwa wazungumzaji wa lugha ya Kirombo ambao wanajifunza Kiswahili kama lugha ya pili ilhali utafiti huu umechunguza kipengele cha mofolojia kwa kubainisha maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyopo katika lugha ya Kisiha, kwa upande wa fonolojia tumeonesha athari za sauti za Kiswahili katika lugha ya Kisiha.

3. Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulitumai mbinu mbalimbali katika kukusanya na kuchambua data za utafiti kuhusu athari za kimofonolojia za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha. Utafiti ulifanyika katika wilaya ya Siha, mkoa wa Kilimanjaro, hususan katika kata za Nasai na Livishi, katika vijiji vya Nraokisangara na Samakimaini, vilivyochaguliwa kutokana na kuwa na wazungumzaji asilia wa Kisiha na ukaribu wa kijiografia uliorahisisha upatikanaji wa data. Mada ya kuathiriana kwa lugha ni pana, hivyo utafiti ulijikita katika fonolojia na mofolojia pekee. Sampuli ya utafiti ilihusisha watoa taarifa 60, wakiwemo wanafunzi 40 wa darasa la tano na la sita kutoka shule za msingi Maarabo na Samaki walioteuliwa kwa usampulishaji kusudio, pamoja na wazee 20 wenye umri wa miaka 50–85 walioteuliwa kwa usampulishaji tajwa. Mbinu kuu za ukusanyaji wa data zilikusishwa hojaji nusu-funge, mahojiano ya ana kwa ana, na ushuhudaiji wa moja kwa moja, zikisaidiwa na vifaa kama michoro, simu ya kiganjani, shajara, na kompyuta pakatwa. Data zilipatikana kupitia uandishi wa hadithi fupi, maelezo ya picha, mazungumzo yaliyorekodiwa, na uchunguzi wa matamshi shuleni na nyumbani. Uchambuzi wa data ulifanyika kwa mkabala wa kimaalezo, ukihusisha tafsiri ya taarifa katika Kiswahili, upangaji wake katika majedwali, na ufafanuzi wa kina unaoongozwa na Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles (1982) ^[12], ili kueleza kwa ufasaha mitazamo na uzoefu wa watoa taarifa kuhusu athari za Kiswahili katika lugha ya Kisiha.

4. Matokeo Na Mapendekezo

4.1. Muhtasari wa Utafiti

Tasinifu hii imegawanywa katika sura tano. Sura ya kwanza inahusu vipengele vya utangulizi kuhusu lugha ya Kisiha, eneo la utafiti, usuli wa tatizo la utafiti na tamko la utafiti. Aidha, malengo ya utafiti yamewekwa bayana ambapo kuna lengo kuu na malengo mahususi na maswali ya utafiti. Vilevile, umuhimu wa utafiti, mpangilio wa tasiniifu pamoja na mawanda ya utafiti vimejadiliwa katika sura hiyo.

Sura ya pili, imeelezea kwa kina mapitio ya machapisho kuhusu mada ya utafiti. Mapitio hayo yamegawanywa katika sehemu ndogondogo tatu ambazo ni mapitio kuhusu dhana muhimu zilizotumika katika utafiti huu kama vile maneno, fonolojia na mofolojia. Aidha, mapitio kuhusu kuathiriana kwa lugha kwa ujumla pamoja na athari za lugha mbalimbali yamemakinikia tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalamu. Katika tafiti hizo, imebainika kuwa lugha huweza kuathiriana katika vipengele vya mofolojia, fonolojia, sintaksia na semantiki.

Zaidi ya hayo, sura imeangazia nadharia iliyotumika ambayo ni Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles (1982)^[12]. Nadharia hii imetumika kwa vile inaeleza kuwa mwingiliano wa wanajamii kutoka katika sehemu mbalimbali kwa sababu za kiuchumi, kisiasa na kijamii husababisha lugha kuathiriana katika matumizi ya maneno na sauti. Hivyo, nadharia hii imesaidia kuonesha ni kwa namna gani jamii ya Wasiha wanazungumza Kiswahili kutokana na kuingiliana katika shughuli mbalimbali hususan biashara na elimu.

Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti zilizotumika katika mchakato mzima wa kukusanya na kuchambua data. Katika sura hiyo, eneo la utafiti, mawanda ya utafiti usampulishaji na mbinu za uteuzi wa sampuli, njia za kukusanyia data ambazo ni hojaji, mahojiano na ushuhudiaji vimeelezewa. Aidha, vifaa vya utafiti vilivyotumika katika kukusanya data ambavyo ni michoro, simu, shajara na kompyuta pakatwa. Vilevile, mkabala uliotumika katika uchanganuzi wa data pamoja na kipengele kinachohusu maadili ya utafiti vimefafanuliwa.

Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data ambazo zilikusanywa kwa njia za ushuhudiaji, mahojiano na hojaji. Data hizo zimechambuliwa kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles (1982)^[12]. Hivyo, matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa lugha ya Kisiha imeathiriwa na lugha ya Kiswahili kwani baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kisiha hususan wanafunzi wanachanganya sauti na maneno ya lugha ya Kiswahili wakati wanapozungumza Kisiha. Sura ya tano inahusu muhtasari wa utafiti, matokeo pamoja na mapendekezo ya tafiti fuatishi.

4.2. Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kuna maneno ya lugha ya Kiswahili ambayo hutumiwa na wazungumzaji wa lugha ya Kisiha. Mtafiti alibaini maneno hayo katika hadithi zilizotungwa na watoa taarifa pamoja na kufafanua michoro mbalimbali waliyopewa kwa kutumia lugha ya Kisiha. Kutokana na uchunguzi wa kazi hii, tulibaini kuwa nomino za Kiswahili ni maneno ambayo yalitumiwa ikilinganishwa na vielezi, vitenzi, vivumishi na viunganishi. Nomino zimetumiwa kwa sababu kuna uchanganyaji wa maneno kutoka katika lugha ya Kiswahili na kutumiwa katika lugha ya Kisiha. Aidha, katika data tulizozipata uwandani tuligundua kuwa baadhi ya nomino zilizotumiwa na watoa taarifa kama vile redio, simu, televisheni, mpira, nyanya na simba ni maneno ya Kiswahili ambayo hayana visawe katika lugha za Kisiha. Hivyo, wazungumzaji wa lugha ya Kisiha hutumia maneno hayo kama yalivyo katika Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yanafanana na matokeo ya tafiti za Mukuthuria (2004)^[43] na Lusanja (2014)^[27] ambapo wameonesha kuwa katika Kitigania na Kiwanji kuna maneno ya Kiswahili na kategoria iliyotumika kwa kiasi kikubwa ni nomino ambazo zimetokana na kukopwa kutoka katika lugha nyingine. Katika utafiti huu, tumebaini kuwa kuna matumizi

ya maneno ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha ambapo nomino zilizotumika ni kutokana na kutokuwa na visawe vya nomino hizo katika lugha ya Kisiha.

Vilevile, kutokana na matokeo ya utafiti huu tumegundua kuwa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyotumiwa na watoa taarifa yana visawe vyake katika lugha ya Kisiha. Hivyo, imebainika kuwa baadhi ya wazungumzaji wake wanatumia maneno ya lugha ya Kiswahili ilhali visawe vyake katika lugha ya Kisiha vipo. Hali hii, inatudhihirishia jinsi Nadharia ya Makutano na Mwachano ilivyo faafu kwani Wasiha wameiacha lugha yao ya Kisiha na kutumia Kiswahili suala ambalo husababisha watoto na vijana kushindwa kutumia lugha ya Kisiha kwa ufasaha. Hivyo, kutokutumika kwa lugha ya Kisiha hasa kwa watoto na vijana ni dalili ya kupoteza wazungumzaji mahiri wa lugha ya Kisiha.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yamebaini kuwa lugha ya Kisiha imeathiriwa na lugha ya Kiswahili katika baadhi ya sauti zake. Imebainika kuwa sauti hizo zilivyokuwa zinatumiwa zamani siyo sawa na zinavyotumiwa hivi sasa. Matokeo yamebaini kuwa

watoa taarifa wanafunzi walitumia sauti za lugha ya Kiswahili badala ya kutumia sauti za lugha ya Kisiha. Kwa mfano, watoa taarifa wanafunzi walitumia sauti [m] badala ya kutumia sauti [n], sauti [z] badala ya kutumia sauti [s] na sauti [p] badala ya kutumia sauti [b]. Hivyo, watoa taarifa wanafunzi wamebainika kuathiriwa zaidi na sauti za lugha ya Kiswahili ilhali wazee wanatumia sauti husika katika lugha ya Kisiha. Kwa hiyo, matokeo ya lengo la pili ambalo ni kueleza athari za kifonolojia za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kisiha yanaonesha jinsi Nadharia ya Makutano na Mwachano ya Giles (1982)^[12] ilivyo mwafaka kwa sababu inajaribu kuonesha namna ambavyo wazungumzaji wa lugha ya Kisiha wanavyoathiriwa na sauti za lugha ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine, tumebaini athari iliyojitokeza ni udondoshaji wa sauti katika baadhi ya maneno ya lugha ya Kisiha. Utafiti umebaini kuwa kuna udondoshaji wa sauti [h] katika baadhi ya maneno ya lugha ya Kisiha. Udondoshaji huo hutokea kutokana na watoa taarifa wanafunzi kutokujua matamshi sahihi ya lugha ya Kisiha.

Katika utafiti huu tumebaini kuwa kuna sababu mbalimbali zinazochangia lugha ya Kiswahili kuathiri lugha ya Kisiha. Miongoni mwa sababu hizo ni elimu, biashara na upanuzi wa matumizi ya Kiswahili vijijini. Nadharia hii ya Makutano na Mwachano ya Giles (1982)^[12] imefanikisha kufikia kupata matokeo ya utafiti huu kwa kuwa inaweka bayana mambo yanayosababisha jamiilugha fulani kukubali kutumia na kuathiriwa na jamii lugha nyingine.

4.3. Mchango wa Utafiti

Kuathiriana kwa lugha moja na nyingine ni eneo ambalo limeamsha ari kwa wataalamu mbalimbali wa lugha kuendelea kuichunguza lugha. Uchunguzaji huo umejikita katika ngazi mbalimbali kama vile fonolojia, mofolojia, semantiki na sintaksia. Miongoni mwa wataalamu hao ni Rubanza (1979)^[46], Mochiwa (1979)^[39] Massamba (1986)^[29] na Lusanja (2014)^[27] waliofanya tafiti kuhusu kuathiriana kwa lugha ya Kiswahili na lugha za Kibantu. Aidha, matokeo ya tafiti zao yalionesha sababu za lugha za Kibantu kama Kihaya, Kizigua na lugha za Mara kuathiriwa na Kiswahili. Matokeo ya tafiti hizo yaliweka bayana sababu ambazo zimejiegemeza katika taaluma ya isimu jamii ambazo ni elimu, uhamiaji, biashara, na wingilugha. Aidha, katika utafiti huu baadhi ya sababu zilizobainishwa zinafanana na

sababu zilizotolewa na watafiti waliotangulia. Aidha, utafiti huu, ni tofauti na tafiti zilizotangulia kwani umechunguza athari za Kimofofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha, hususan katika kubainisha maneno ya lugha ya Kiswahili yaliyomo katika lugha ya Kisiha kwa kuyagawa katika kategoria mbalimbali za maneno kama nomino, vivumishi na vielezi. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa athari za lugha zinaweza zikajitokeza katika ngazi ya mofofonolojia, kwa kuzingatia kigezo cha matumizi ya maneno.

Aidha, matokeo ya utafiti huu yana mchango katika jamii ya Wasihia kwani kwa kurejelea sampuli iliyotumika ya wazee na wanafunzi ni wazi kuwa wanafunzi wameathiriwa na lugha ya Kiswahili kutokana na mfumo wa elimu unaosisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili kuliko Kisiha. Hivyo, kutokana na matokeo hayo ni wazi kuwa Kisiha kinapotea hasa kwa watoto kutokana na kutokukitumia katika maeneo rasmi kama shuleni, mahakamani na hospitalini. Hivyo, utafiti huu unatoa mchango kwa kuhimiza jamii ya Wasihia kutumia lugha kwa kuwa jamii ndiyo yenye jukumu la kudumisha na kuiendeleza lugha katika miktadha mbalimbali.

5. Hitimisho

Sura hii imejadili muhtasari wa utafiti kwa kuonesha kuwa utafiti huu umegawanywa katika sura kuu tano. Aidha, matokeo ya utafiti kuhusu athari za kimofofonolojia za Kiswahili katika lugha ya Kisiha yamefafanuliwa. Sura hii pia imetoa mapendekezo ya tafiti fuatishi zinazoweza kufanywa kuhusu kuathiriana kwa lugha.

6. Marejeleo

- Adriaans N, Blanken P, Hendricks VM. Snowball sampling: a pilot study on cocaine use. Rotterdam: IVO; 1992.
- Arab S. Effect of French in teaching and learning English [master's thesis]. Tlemcen: Chuo Kikuu cha Tlemcen; 2015. Unpublished.
- Baker MC. Lexical categories. Cambridge: Cambridge University Press; 2003.
- Batibo HM. Language endangerment and death in Africa: causes, consequences and challenges. Clevedon: Multilingual Matters; 2005.
- Bosha I. Athari ya Kiarabu katika Kiswahili Sanifu [doctoral dissertation]. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 1993. Unpublished.
- Bryman A. Social research methods. 4th ed. Oxford: Oxford University Press; 2004.
- Chiduo EKF. Kiswahili katika Elimu. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 1999.
- Chimera RM. Kiswahili through ages, the question of lexicon. Egerton: Egerton University; 1999. Unpublished.
- Cohen L, Manion L, Morrison K. Research methods in education. London: Routledge; 2000.
- Dressler WU. Language death. In: Newmeyer FJ, editor. Linguistics: the Cambridge survey IV. Cambridge: Cambridge University Press; 1988. p. 184-91.
- Enon CJ. Education research statistics and measurement. Kampala: Makerere University; 1998.
- Giles H, Byrne JL. An intergroup approach to second language acquisition. *J Multiling Multicult Dev.* 1982;19(3):17-40.
- Guthrie M. Second prehistory of the Bantu languages. UK: Gregg International Publishers; 1948.
- Hooper J. Introduction to generative phonology. Oxford: Oxford University Press; 1976.
- International Phonetic Association. Handbook of the International Phonetic Association. Cambridge: Cambridge University Press; 2005.
- Kadenge M. The influence of Shona phonology on the English speech of first language [doctoral dissertation]. Harare: Chuo Kikuu cha Zimbabwe; 2003. Unpublished.
- Kapinga MC. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: TUKI; 1983.
- Katamba F. An introduction to morphology. London: Macmillan; 1993.
- Khamis M. Athari za Matamshi ya Msamiati wa Kiswahili Sanifu katika Kimakunduchi [master's thesis]. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 2012. Unpublished.
- Kihore YM, Massamba DPB, Msanjila YP. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA). Dar es Salaam: TUKI; 2003.
- Kitito KO, Makombo HS, Med'hi ES. Ana kwa Ana na Kiswahili: kitabu cha mwanafunzi. Nairobi: Abantu Publication; 2009.
- Kombo DK, Tromp DLA. Proposal and thesis writing. Nairobi: Paulines Publications Africa; 2006.
- Kothari CR. Research methodology: methods and techniques. 2nd rev. ed. New Delhi: New Age International Publishers; 2004.
- Kothari CR. Research methodology: methods and techniques. New Delhi: New Age International Publishing Ltd; 2008.
- LOT. Atlasi ya Lugha za Tanzania. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 2009.
- Luka E. Mwingiliano wa Matumizi ya Lugha baina ya Kiswahili na Kimeru na Athari zake katika Lugha hizo [master's thesis]. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 2012. Unpublished.
- Lusanja SU. Athari za Kiswahili katika Msamiati wa Kiwanji [master's thesis]. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 2014. Unpublished.
- Maho JF. The online version of the new updated Guthrie list (NUGL): a referential classification of the Bantu languages [Internet]. 2009 [cited 2015 Nov 11]. Available from: <http://goto.glocanet/mahopapers/nuglionline.pdf>
- Massamba DPB. On the influence of local languages on Kiswahili: the case of Mara region in Tanzania. *Kiswahili.* 1986;53(1-2).
- Massamba DPB, Kihore YM, Msanjila YP. Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA): sekondari na vyuo. Dar es Salaam: TUKI; 2004.
- Massamba DPB. Phonological theory: history and development. Dar es Salaam: TUKI; 2010.
- Massamba DPB. Maendeleo ya Nadharia ya Fonolojia. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 2011.
- Martens DM. Research methods in education and psychology: integrating diversity with quantitative and qualitative approach. London: SAGE Publications; 1998.
- Mediesson I. Patterns of sound. USA: Cambridge University Press; 2005.
- Mekacha RDK. Isimujamii: nadharia na muktadha wa Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI; 2011.

36. Mgullu RS. Mtaala wa Isimu. Nairobi: Longhorn Publishers; 1999.
37. Mligo ES. Jifunze Utafiti: mwongozo kuhusu utafiti na uandishi wa ripoti wenye mantiki. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering (EGYS); 2012.
38. MLUTA. Atlas ya Lugha za Tanzania. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 2009.
39. Mochiwa ZSM. The impact of Kiswahili ethnic language: a case study from Handeni district [doctoral dissertation]. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam; 1979. Unpublished.
40. Mramba PT. Uchunguzi wa Athari za Kirombo katika Ujifunzaji wa Kiswahili [master's thesis]. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 2015. Unpublished.
41. Msanjila YP. The use of Kiswahili in rural areas and its implications for the future of ethnic language in Tanzania [doctoral dissertation]. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; 1999. Unpublished.
42. Msanjila YP. Isimujamii: sekondari na vyuo. Dar es Salaam: TUKI; 2009.
43. Mukuthuria M. Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru [doctoral dissertation]. Njoro: Chuo Kikuu cha Egerton; 2004. Unpublished.
44. O'Grady W, Dobrovolsky M, Katamba F. Contemporary linguistics. London: Longman; 1997.
45. Ogden R. An introduction to English phonetics. Edinburgh: Edinburgh University Press Ltd; 2009.
46. Rubanza YI. The relationship between Kiswahili and other African languages: a case study Kihaya [doctoral dissertation]. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam; 1979. Unpublished.
47. Rubin HJ, Rubin IS. Qualitative interviewing: the art of hearing data. London: Sage Publications; 1995.
48. Spencer A. Morphological theory: an introduction to word structure in generative grammar. Basel: Blackwell; 1991.
49. Thomason SG. Language contact. Edinburgh: Edinburgh University Press; 2001.
50. Tripathi PC. A textbook of research methodology in social sciences. New Delhi: Sultan Chand and Sons Publishers; 1991.
51. TUKI. Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha. Dar es Salaam: TUKI; 1990.
52. TUKI. Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Oxford University Press; 2004.
53. TUKI. Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Dar es Salaam: Oxford University Press; 2013.
54. Vogt WP. Dictionary of statistics and methodology: a nontechnical guide for the social sciences. London: Sage; 1999.
55. Wamitila KW. Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi. Nairobi: Focus Publishers; 2011.
56. Zawawi K. Loan words and their effect on the classification of the Swahili nominals: a morphological treatment. New York: Columbia University; 1979.

SA 4.0) License, which allows others to remix, tweak, and build upon the work non-commercially, as long as appropriate credit is given and the new creations are licensed under the identical terms.

How to Cite This Article

Kileo JG. Athari Za Kimofonolojia Za Kiswahili Katika Lugha Ya Kisiha. *J Front Multidiscip Res*. 2025;6(2):315–23.

Creative Commons (CC) License

This is an open access journal, and articles are distributed under the terms of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International (CC BY-NC-